Ukweli Hauna Kutu

# Pambazuko

Toleo Namba 013 | Jumatatu Oktoba 3-10, 2022

Uk. 12: Samia ateua mawaziri



## ‘Ndoto za Alinacha’ Sekta ya Utalii

- *Wadau washauri makubwa kukwamua*

Una mimba? Tafuna karanga - Uk. 18

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

# Nani awalinde watoto wetu?

MIAKA 13 iliyopita, Tanzania haikuwa na sheria ya mtoto, hivyo kila jamii, kabila na hata ukoo, ilikuwa na tafsiri yake kuhusu haki na taratibu za kuishi na kundi hilo linaloweza kutajwa kuwa ni maalum kwa kuwa lina watu wenye umri mdogo – wengi wakiwa na akili zisizokuwa pevu.

Pamoja na mtambuka huo wa haki na taratibu za kulea kundi hilo, makabila, koo na jamii zote za Tanzania zilikuwa na kazi kubwa ya kulinda maisha ya watoto, ili 'yasivurugwe' kwa maana ya kuwalinda ili nao 'wasivuruge' wanapokuwa wakubwa.

Ni kutokana na mtazamo huo, makabila, koo, na jamii nyingi – tangu enzi na enzi, zilikuwa zikiwatenga katika kazi, kula, kulala, mafunzo na hata kwenye mazungumzo rasmi ya wakubwa. Watoto walikuwa na maeneo yao maalum ya kufanya vitu vyao.

Jamii hizo za kale, zilikuwa zikiwalinda watoto na makundi ya watu wenye umri mkubwa na zaidi sana ikiwapa elimu ya kuepukana na makundi ya vijana wasiokuwa na maadili, wazembe wa kazi za nyumbani na shamba na wavuta bangi.

Kuja kwa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 ilikuwa ni kutimiliza yale yaliyokuwa yakifanywa na jamii hizo za kale na kwa kuzingatia mazingira ya Tanzania na mikataba mingine ya kimataifa. Kamwe sheria hiyo haikuwa na jambo geni, isipokuwa tu kutaja umri wa mtoto kwamba ni yule mwenye miaka chini ya 18.

Sheria hii ambayo pia imechota maeneo kadhaa kwenye sera ya taifa ya watoto, inaweka bayana muundo unaolenga kumpa mtoto kinga pamoja na viwango kwa ajili ya utoaji haki kwa watoto, na pia kuweka misingi ya kulindwa dhidi ya maonevu yoyote na kwa namna yoyote ile.


Kwamba kila mtu ana haki na wajibu wa kulinda haki za mtoto na kudhibiti kila kinachoonekana kuingilia uhuru wake ili kumjengea mazingira bora ya kuwa Mtanzania mwema na kuwajibika kwa ajili yake, familia na hata maendeleo ya taifa.

Ni dhahiri kwamba malezi wanayopewa watoto ndiyo msingi wa mustakabali wao. Maisha ya mtu hutegemea sana msingi wa malezi aliyopata tangu angali mtoto.

Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa sheria hiyo, bado jamii ya sasa imegeuka kuwa katili mno dhidi ya maisha ya watoto. Idadi ambayo haifahamiki kirahisi – waliokuwa watoto wakati sheria hiyo inatungwa, wamekuwa vijana watukutu wakiwamo vibaka, wezi, majambazi, watumia dawa za kulevya na wenye kufanya biashara ya kuuza miili yao kwa ngono.

Kimsingi, mtoto hazaliwi akiwa na tabia mbaya. Hufunzwa na jamii inayomzunguka kwa njia mbalimbali. Wapo wanaopata tabia hizo ndani ya familia kutoka kwa wakubwa zao, kutoka shuleni, kutoka kwenye nyumba za ibada na kwa majirani.

Swali la kujiuliza, je, nani tumwamini kulea watoto ikiwa hata wazazi wanashiriki kuharibu mustakabali wa watoto wao. Nani tumpe imani ya kutunza watoto ikiwa hata makanisani na misikitini wanarubuniwa na kuvurugiwa maisha? Je, tumpe mwalimu ambaye pia zipo taarifa kwamba nako siyo salama sana kwani wapo walimu wakora. Nani sasa?




## Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: pambazuko1@protonmail.com ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## NUKUU



*"Tunasomesha watoto wetu waje kukariri vilivyoanzishwa ughaibuni, lakini hatuwekezi katika ubunifu. Na mbaya zaidi wanaojaribu kutumia hicho kidogo walichopata huko vyuoni kuanzisha na kumiliki chao, tunawatweza, kuwakatisha tamaa na hata kuwazuia! – Charles Misango, mjumbe wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).*

# TPA kuhamia Dodoma ni mzaha

**Na Asha MABROUK**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA), wiki iliyopita imetangaza kwamba sehemu ya ofisi zake za makao makuu yaliyoko Dar es Salaam, zitahamishia shughuli zake Makao Makuu ya Tanzania, Dodoma.

Pamoja na kwamba taarifa hiyo kwa umma, iliyosambazwa kwenye vyumba vya habari na kufikia pia kwenye mitandao ya jamii, pamoja na kwamba haielezi ni wakuu gani wa mamlaka hiyo watahamia huko, inaelezwa Mkurugenzi Mkuu anaweza kuwa mingoni mwao.

Dalili kwamba mkurugenzi huyo atahamia huko zilianza kuonekana mapema kwani ndani ya jengo ambamo TPA inahamia huko Dodoma – katika Jengo la PSSSF, maarufu kwa jina la Kambarage Tower, ghorofa ya tano, kulielezwa na baadhi ya wahusika kuwa ipo ofisi ya "bosi mkuu."

Tangazo la kuhamia katika jiji hilo linaeleza kuwa kuanzia Septemba 30, 2022 TPA itakuwa huko rasmi.

Pamoja na kupongeza uamuzi wa serikali kuifanya Dodoma kuwa makao makuu ya uhakika ya Tanzania, wengi hawaoni uwepo wa ulazima wa kila ofisi ya serikali kuhamia huko, hata kama shughuli zake, siyo lazima ziwepo huko kutokana na mazingira ya asili ya majukumu.

Inaeleweka kuwa serikali inapenda kuona wakuu wote wa taasisi, mamlaka, mashirika na maeneo nyeti wanakaa jirani na "wakubwa," lakini siyo wote wanapaswa kuwepo huko, hasa kutegemea na kazi zao.

TPA kwa mazingira ya majukumu yake haipaswi kuwepo Dodoma, hasa wakuu wa mamlaka hiyo, kwani wanatakiwa kuwepo – muda wote, kwenye asili ya kazi yao wakisimamia majukumu ipasavyo na siyo kutumia muda mwingi wakiwasiliana kwa "waya" ama maandishi kupitia tarakirishi na vyanzo vingine.



*Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa*

Dodoma hakuna bandari, na haiwezi kuwepo katika hali ya kawaida, hivyo viongozi wa TPA kuwaweka Dodoma ni uamuzi wa kisiasa zaidi badala ya hali halisi.

Katika mitandao ya kijamii wengi wamekuwa wakishangaa uamuzi huo na kueleza namna ambavyo uamuzi huo unaweza kufifisha utendaji kazi wa mamlaka hiyo nyeti yenye jukumu kubwa la kuangalia – kwa ukaribu zaidi, ufanisi na makusanyo ya fedha za kodi kutoka kwa wafanyabiashara wanaoingiza na kusafirisha mizigo kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Kuhamia Dodoma kwa viongozi wa TPA, maana yake ni kuongeza gharama zingine ambazo awali hazikuwepo, kwani wakuu hao watalazimika "kukimbia" mara kwa mara kwenda kwenye kitovu cha shughuli zao ambazo nyingi ziko Dar es Salaam kwa ajili ya ufuatiliaji.

Litakuwa jambo la busara zaidi endapo TPA inaweka, labda ofisi ndogo ya biashara, lakini siyo watendaji wakuu wa mamlaka hiyo ambayo ndiyo 'macho na masikio' ya fungu kubwa la kodi linalokusanywa kupitia bandari zetu, iwe huko.

Inaweza kuhojiwa kwamba "mbona rais hayupo kila mahali na shughuli zinakwenda," lakini siyo bandari ambazo zinatakiwa mara kwa mara kufuatiliwa kwa ukaribu na wakubwa walioaminiwa, badala ya kuangalia utendaji kutoka mbali. Tutapigwa zaidi!

# Wanajeshi waonya mitandao

**Na Mwandishi WETU**

WANAJESHI kote nchini wameonywa kuwa waangalifu wanapotumia mitandao ya kijamii kuwasilisha kitu chochote kwa umma.

Mkuu wa Majeshi Tanzania, Jenerali Jacob Mkunda ametoa onyo – kwa amri ya jeshi akieleza kuwa kila mwanajeshi anapaswa kuwa makini anapotumia mitandao hiyo ya kijamii.

Mitandao anayoizungumzia Jenerali Mkunda ni pamoja na Facebook, Instagram, Twitter, Tik Tok na mingine ambayo sasa ni maarufu duniani kote.

Amesema mitandao ya kijamii, ambayo hutumia simu za mkononi na kompyuta, ni vyema ikatumiwa kwa uangalifu, kwani ikitumika vibaya inaweza kugharimu nafasi ya mhusika.

"Ni marufuku, tukikubaini unatumia mitandao ya kijamii vibaya tutakuchukulia hatua kali, lakini pia mkaishi viapo mlivyoapa kwani mwanajeshi yoyote asiyezingatia kiapo alichoapa hatoshi kuwa mwanajeshi, mmesema mtakuwa waaminifu kwa nchi yenu, mtakuwa watiifu na kuwa wanajeshi hodari, kwa kufanya hivyo mtaona fursa mbalimbali zikifunguka," aliongeza kamanda huyo.

Mkunda aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifunga mafunzo ya awali ya askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ ) sherehe zilizofanyika Kikosi cha 833 KJ Oljoro, mkoani Arusha, huku akisisitiza wahitimu wote kuendelea na nidhamu ya jeshi.

Alibainisha kwamba wapo baadhi ya wanajeshi wasiokuwa na nidhamu, wanatumia mitandao ya kijamii kutukana viongozi wao, kitu ambacho hakikubaliki.

Sambamba na kuonya kuhusu mitandao ya kijamii, Mkunda pia aliwaonya wanajeshi hao kujihusisha na masuala ya siasa ndani na hata nje ya maeneo yao ya kazi.

"Msijihusishe na siasa na hili lipo kisheria, mjue siasa ni sawa na uraibu, ukipenda siasa inakuwa ngumu sana kuacha, hivyo nawaasa acheni kabisa kujihusisha na masuala hayo," alisema.



*Jenerali Jacob Mkunda*

Alieleza kuwa wahitimu hao jukumu lao ni kuhakikisha wanalinda Katiba na uhuru wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, ulinzi wa mipaka, lakini pia kwenda kushiriki katika ulinzi wa amani ya nchi mbalimbali.

Katika kufunga mafunzo hayo ilielezwa kuwa kati ya wahitimu hao 2457; ambapo wanawake ni 606 na wanaume ni 1851, 80 wameshindwa kuhitimu mafunzo hayo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo utoro, ugonjwa, vifo, utovu wa nidhamu, kukosa viwango na sababu zingine ambapo waliohitimu kwa kipindi chote wamelelewa katika maadili na nidhamu za kijeshi.

Mkufunzi Mkuu wa Shule ya Jeshi, Luteni Kanali Joseph Likalangu alisema kuwa wahitimu hao 2457 wamefikia viwango vinavyokubalika na wanaenda kulitumikia taifa kwa moyo mmoja na ujasiri mkubwa, kwani wamepitia mafunzo mbalimbali ikiwemo utimamu wa mwili, ukakamavu na ujasiri.

# Waliopotezana JKT miaka 30 waanza umoja

**Na Mwandishi WETU**

AMA kweli dunia ni duara. Lakini pamoja na uduara wake, kwa mazingira ya sasa ni sawa na kijiji kidogo ambacho hakina mipaka kutokana na maendeleo na ukomavu wa sayansi na teknolojia.

Haya ni maneno yanayoweza kubeba taswira ya umoja ulioanzishwa na Watanzania 140 ambao walikutana mara ya mwisho miaka 30 iliyopita wakilitumikia taifa kwa mujibu wa sheria. Hawa walikuwa kuruta katika Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa Bulombora, mkoani Kigoma.

Walikutana na kuishi kwa mwaka mmoja katika kambi hiyo – kuanzia 1992 hadi 93 walipoachana, huku kila mmoja akirejea kwao. Wengine walirudi kazini na wengine kwenda kuanza masomo vyuoni, hasa elimu ya juu.

Katibu wa umoja huo, ambao umesajiliwa rasmi serikalini, kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani na kuitwa Burombola 92/93, Kitandala Clement anasema kuwa kukutana kwa wanachama wa umoja huo umewezeshwa zaidi na mitandao ya kijamii kupitia simu za mkononi, hasa WhatApp.

"Wazo lilikuja baada ya baadhi yetu kukutana na kuona umuhimu wa kuwa na umoja huo ili kudumisha uhusiano wetu tangu tukiwa kwenye Kambi ya Jeshi Bulombora. Hakika kule tuliishi tukiwa ndugu, ila baada ya kuondoka, tulipotezana, lakini sasa tumekutana tena bila kujali umbali wa maeneo waliko wanachama wetu," anasema Kitandala.

Kitandala anaeleza madhumuni makubwa ya umoja huo ni kuwa wamoja zaidi – kwa wanachama kusaidiana katika shida na raha, kurithisha vipaji na vipawa vya wanachama kwa watoto na pia kuwa na fursa za kuwekeza.

Katibu huyo anasema tangu kuanza kwa umoja huo, miaka karibu miwili iliyopita, wanachama wamekuwa wakiongezeka na kwamba idadi kubwa ya wajumbe wamefaidika kwa misaada ya



*Kitandala*

mawazo na hata rasilimali katika matukio mbalimbali.

Ndani ya umoja huo wa aina yake, kuna wabunge, wakurugenzi, wanajeshi, wafanyabiashara, watumishi wa umma wa kada mbalimbali, wakulima na hata wavuvi.

## Wahafidhina bado waminya uhuru wa habari

**Na Jabir IDRISSA, Dodoma**

PAMOJA na jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan kutoa nafasi kwa vyombo vya habari kufanya kazi zake kwa uhuru, bado kuna mkwamo unaotokana na wahafidhina waliobaki kwenye ofisi za umma kutoka utawala wa Rais John Magufuli.

Hayo yalibainishwa wiki iliyopita na Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, akiwa jijini Dodoma, ambako alisema dunia inaendelea kushuhudia "mkwamo" usiotarajiwa.

"Kwa kiasi kikubwa milango ya kupata na kupasha habari imefunguliwa na Rais Samia; kuna majadiliano yanafanyika sana kiasi cha wale wahafidhina kutoelewa na kutoamini macho yao, kwamba ubabe waliozoea kuminya vyombo vya habari, sasa unaonekana kukemewa," anaongeza Kajubi.

Anasema dunia ilishangaa pale Rais Samia alipotoa tamko la kufungulia vyombo vyote vilivyokuwa vimefungwa, lakini watendaji wa sekta ya habari wakatoa kauli za kuonesha waliofunguliwa ni vyombo vya mitandao tu.

# Kumbukizi ya miaka 23


## ya kifo cha Baba wa Taifa

Gazeti la Pambazuko la Oktoba 10, 2022 litakuwa toleo maalum kwa ajili ya kukumbuka kazi zilizotukuka za Mwalimu Nyerere, kabla ya uhuru, wakati wa kupigania uhuru, uongozi wake, kustaafu na hadi kifo.

Hivyo, ukiwa mdau na msomaji wa Pambazuko tunakualika kutuma tangazo lako lenye maudhui yenye kuonyesha namna wewe, kampuni, shirika au taasisi yako inavyomkumbuka mwana huyo wa Tanzania na Afrika.

Tuma tangazo lako kwa barua pepe; advertisement@pambazuko.tz au piga simu: 0744 768273 ili kuhudumiwa.

Tanzania na dunia itafurahi kuungana pamoja kumkumbuka Mwalimu Nyerere aliyefariki dunia Oktoba 14, 1999.



# Mgawanyiko wa mamlaka

**Na Askofu Stephen MUNGA**

HAIWEZEKANI kuzungumza juu ya umiliki wa taifa pasipo kuzungumzia mgawanyiko wa mamlaka.

Ieleweke kuwa siasa katika nyakati hizi ni hasa juu ya mgawanyiko wa mamlaka ili kuwezesha utoaji haki na utoaji wa huduma muhimu kwa jamii.

Fikra za kisiasa au utendaji wa kisiasa, kwa kila wakati unapaswa kuzingatia na kuendana na namna ya uelewa juu ya haki ulivyojengeka na ufanisi wa mfumo mzima wa ustawi kwa ajili ya kuongeza ubora wa maisha ya raia.

Baada ya ukoloni, mataifa mengi yaliyopata uhuru 'yalikimbilia' kujenga miundo na mifumo mipya ya utawala ambayo ingeongeza haki na kuhakikisha ufanisi katika ujenzi wa ustawi wa watu.


Kiini cha juhudi hizo ilikuwa kudhihirisha kwa maneno na vitendo kwamba kuwa huru maana yake ni kuweka umiliki wa taifa na mamlaka mikononi mwa watu.

Hata hivyo, inasikitisha kwamba matokeo ya juhudi hizi hayajawa ya mafanikio katika nchi nyingi zilizokuwa chini ya ukoloni

Kwa uelewa huo wa mgawanyiko wa mamlaka kwa nyakati hizi - na bila shaka kwa nyakati zijazo, una malengo hayo. Kwa hiyo basi ni juu ya watawala siku zote kuweka sikio lao kwa jamii ambayo ndio wenye taifa na ndio wenye madaraka ili kujua ni nini jamii inahitaji kwa kila nyakati. Kwa serikali iliyo ya watu inayoongozwa kwa matakwa ya watu haiwezi kupuuza sauti za watu.

Mgawanyiko wa mamlaka ulio na ufanisi - mara zote, utakuwa na uwezo wa kubadilika na kubadilisha mambo kulingana na mahitaji ya jamii.

Viongozi wanapaswa kuwa na maono ya uongozi wao, lakini hayo yaweza kutekelezwa kwa mafanikio pale tu yanaporandana na matakwa ya watu. Kwa hiyo, kimsingi kulingana na nadharia hii, wanaoamua juu ya mwelekeo wa taifa ni watu na wala siyo watawala.



*Mwl. Nyerere*

Hii ndio sababu bunge kama chombo kinachowakilisha watu, lina nafasi kubwa katika kudhihirisha dhamira ile kwamba mamlaka imo mikononi mwa watu.

Mabadiliko yanayoendana na kubadika kwa matakwa ya watu kulingana na nyakati yanakuja na mambo mengi. Miongoni mwa hayo ni mabadiliko ya sheria na wakati mwingine mabadiliko ya katiba ya nchi.

Suala la mabadiliko ya sheria na ikibidi mabadiliko ya katiba siyo matakwa au hiari ya watawala bali ya watu. Vilevile mabadiliko hayo yanaweza kudai mabadiliko ya watawala na kufumua miundo na mifumo ya utawala ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mambo kwa malengo ya kuboresha maisha ya watu.

Pale ulipo utawala bora suala la mabadiliko ya katiba na sheria kwa manufaa ya jamii siyo jambo la kuvutana, bali la kuunganisha watawala na watawaliwa walio wamiliki wa taifa katika safari moja ya kuboresha maisha ya jamii.



## Mezani kwa Chahali

**Na Evarist Chahali**
evarist@chahali.com

# Gumzo la vijana na vumbi la Kongo

MIONGONI mwa habari zilizotawala wiki iliyopita ni agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kwamba kufanyike utafiti wa kwanini vijana-balehe wanakuwa na lishe ndogo na hafifu, wakati taifa linahitaji vijana wenye nguvu kwa maendeleo ya taifa.

"Mara wengine wanahangaika na vumbi la Kongo, mara kitu gani, lakini tatizo kubwa liko kwenye lishe," alisema mkuu huyo wa nchi.

Hata hivyo, kauli hiyo ilizua mjadala kwenye mitandao ya kijamii. Kwa upande mmoja, kuna waliohoji kama agizo hilo la Rais Samia lilikuwa na uzito zaidi ya mjadala mkali unaoendelea kuhusu Jeshi la Polisi kugubikwa na madai ya kuua watu watatu wanaotuhumiwa kuwa majambazi.

Kilichogusa hisia za watu wengi kuhusu mauaji hayo ni taarifa kwamba binti wa mmoja wa watu waliouawa alilazimishwa kufanya tendo la ndoa na baba yake.

Kwa upande mwingine, kuna waliodai tatizo alilogusia Rais Samia linachangiwa zaidi na sababu za kiuchumi. Kwamba ugumu wa maisha unawafanya vijana wawe na lishe duni ambayo nayo husababisha upungufu kwenye afya yao ya uzazi, kwa mfano upungufu wa nguvu za kiume.

Kadhalika, kuna hisia kwamba baadhi ya vijana hukimbilia "vumbi la kongo" au pweza (ili kuongeza nguvu za kiume) kwa imani kwamba kutokana na "nguvu zao haba kiuchumi", njia pekee ya kudumisha uhusiano wa kimapenzi ni kuwaridhisha wenza wao.

Hisia hiyo inaambatana na nyingine kwamba "katika Tanzania ya sasa, uwezo wa kiuchumi ni kigezo muhimu katika kudumu au kudhoofika kwa uhusiano wa kimapenzi".



*Rais Samia Suluhu Hassan*

"Vijana wakiwa na nguvu za kiuchumi hakutokuwa na haja ya kuhofia kuhusu nguvu za kiume," alidai mwanasiasa mmoja wa upinzani.

Kwa mtazamo wangu, kama Rais Samia alipaswa kuongelea tuhuma dhidi ya Jeshi la Polisi, au tuhuma za udhalilishaji aliofanyiwa binti mmoja wa waliouawa, au hakupaswa - ni suala linalojadilika, lakini pia ni muhimu kutambua kuwa "Rais hapangiwi cha kuongea," japo hili nalo linajadilika.

Kwa kuendelea nilichogusia katika makala iliyopita, mbinu mbalimbali za "jinsi ya kuwa mtu bora" zinaweza kuwa na msaada kukabili changamoto za afya ya uzazi, ikiwa ni pamoja na upungufu wa nguvu za kiume.

Tahajudi (meditation) kwa mfano, inaweza kuwasaidia vijana wanaotumia muda mwingi kuangalia filamu za ngono, ambazo mara nyingi husababisha wao kujichua, tendo linalodaiwa kuchangia kwa kaisi kikubwa kupungua kwa nguvu za kiume.

# ‘Ndoto za Alinacha’ Sekta ya Utalii

**Na Waandishi WETU**

MALENGO ya Tanzania kuwa kinara wa utalii katika ukanda wa Afrika, huenda yakabaki kuwa “ndoto za Alinacha” pamoja na mikakati inayowekwa na serikali.

Sababu kubwa ya kushindwa kufikia malengo yake ni kukwama kupanga mikakati na mbinu za kuvutia zaidi watalii kutoka nchi zenye watu wanaopenda kutembelea vivutio, hasa vinavyopatikana Afrika, Tanzania ikiongoza.

Hata hivyo, pamoja na kuongoza kwa vivutio vingi, ikiwamo mbuga na hifadhi zenye wanyama anuai wa kuvutia, mlima mrefu kuliko yote Afrika; Mlima Kilimanjaro, vivutio vilivyoko Zanzibar, ikiwamo fukwe na malikale, bado Tanzania inazidiwa idadi ya watalii na nchi zenye idadi ndogo ya vivutio.

Tanzania ndiyo inayoongoza duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya wanyama kwa kila mita ya eneo.

Taarifa zilizopatikana zinaeleza kwamba Tanzania imepanga kufikisha watalii milioni 25 kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

Pambazuko limedokezwa na wadau wa sekta ya utalii, wachumi na wanazuoni wengine kwamba idadi ya watalii milioni tano kila mwaka haiwezi kufikiwa kwa mikakati ya sasa, ikiwamo hata kutangaza nchi kupitia filamu ya Royal Tour “iliyoongozwa” na Rais Samia Suluhu Hassan.

“Idadi ya watalii milioni tano kila mwaka, bado ni mtihani mkubwa, kwani bado jitihada zinazofanywa na taasisi, mamlaka na bodi za sekta hiyo, zinaonekana kusuasua,” anasema Hans Holmes, mtaalam wa utalii kutoka Ujerumani.

Hans ambaye amejitambulisha kuwa shabiki wa utalii wa Tanzania, anaseme serikali bado haijaweka nguvu za ziada kukusanya mapato makubwa ya utalii, ingawa fursa zipo.

Kutokana na idadi ya watalii milioni 5 kila mwaka, Tanzania ililenga kukusanya mapato yanayofikia dola za Marekani bilioni 6, sawa na Sh. 1,380,000,000,000,000 (Trilioni 1.38) kwa ujio wa watalii hao.

Watalii milioni tano kwa mwaka, ni sawa na asilimia 21 ya watalii waliopatikana kwa miaka mitano, yaani tangu 2015 hadi 2019, katika nchi zote tano za Mauritius, Afrika Kusini, Botswana, Kenya na Tazania zilizopokea watalii 104,182,000.

Aidha, mapato ya dola bilioni 6 ni makubwa mara 14 ya dola 428,968,030, ambayo ni mapato ya Tanzania katika sekta ya utalii kwa miaka mitano iliyopita, kati ya mwaka 2017 hadi 2022.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Maendeleo ya Sekta ya Utalii Duniani kwa mwaka 2021, kama ilivyoandaliwa na Jukwaa la Uchumi Duniani (WEF), na chapishwa Mei 2022, Tanzania ni miongoni mwa nchi kumi zenye maendeleo mazuri kwenye sekta ya utalii, ndani ya Ukanda wa Afrika ya Kusini mwa Jangwa la Sahara (SSA).

Nafasi za kwanza hadi ya nne zimechukuliwa na Mauritius, Afrika Kusini, Botswana na Kenya. Tanzania inakalia nafasi ya tano. Nafasi za sita hadi kumi zimechukuliwa na Cape Verde, Namibia, Rwanda, Zambia na Ghana. Kwa hiyo, wababe wa Tanzania ni Mauritius, Afrika Kusini, Botswana na Kenya.

Kulingana na takwimu za watalii wa kimataifa zilizotangazwa na Benki ya Dunia, Septemba 16, 2022, kwa miaka

# ‘Ndoto za Alinacha’ Sekta ya Utalii

*Inatoka Uk. 10*

mitano iliyopita, yaani tangu 2015 hadi 2019, nchi tano za Mauritius, Afrika Kusini, Botswana, Kenya na Tazania zilipokea watalii 104,182,000.

Kati ya watalii hawa, Mauritius ilipokea watalii 6,701,000, sawa na asilimia 6.4; Tanzania watalii 6,781,000 sawa na asilimia 6.5; Kenya watalii 8,044,000, sawa na asilimia 7.7; Botswana watalii 8,807,000, sawa na 8.5; na Afrika Kusini watalii 73,849,000, sawa na asilimia 70.9.

Kwa hiyo, endapo Tanzania ina ndoto ya kuwa kiranja mkuu wa utalii bora Kusini mwa Afrika, inapaswa kuongeza idadi ya watalii wa kimataifa mara 11 ndipo ifanikiwe kuipiku Afrika Kusini. Huu ni mtihani mkubwa.

Wadau wa utalii wanaeleza kuwa kusudi idadi ya watalii wanaoingia nchini iendelee kuongezeka zaidi ya idadi ya watalii waliorekodiwa kabla ya janga la Covid-19, Tanzania italazimika kuongeza juhudu za kimkakati ili kuweza kuvutia watalii wengi zaidi.

Hata hivyo, ili kufikia malengo hayo ya juu Tanzania itahitaji mkakati maalum unaozingatia “vipaumbele kwa ajili yakukuza sekta ya utalii.”

Wadau hao wanavitaja vipaumbele hivyo kuwa ni pamoja na kufika kwenye vivutio kwa urahisi – barabara, viwanja vya ndege na bandari, malazi - yaani, hoteli zenye huduma bora; uwepo wa huduma kama vile intaneti na maduka makubwa; bei rafiki kwa wageni kuishi na kutembelea maeneo mengi, usalama wao, huduma zenye hadhi za juu na kuongeza bajeti ya kutangaza utalii nje ya Tanzania.



*Moja ya vivutio ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, iliyoko Tanzania, ni uwepo wa idadi kubwa ya viboko katika maji yanayoungana kutoka mito ya Seronera na Orangi. Watalii wengi, wa ndani na nje, hufika kuona maisha ya wanyama hao - (Picha kutoka TTB).*

*Inaendelea Uk. 12*

# Samia ateua mawaziri

**Na Mwandishi WETU**

Rais Samia Suluhu Hassan amefanya mabadiliko madogo kwenye Baraza la Mawaziri jana Oktoba 2, 2022.

Katiba mabadiliko hayo, Rais amemteua Dk. Stergomena Lawrence Tax kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Awali Dk. Tax alikuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Dk. Tax anachukua nafasi ya Balozi Liberata Mulamula.

Taarifa iliyotolewa jana usiku na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu haikueleza Balozi Mulamula anakwenda kushika nafasi gani.

Aidha, Rais amemteua Innocent Lugha Mashungwa kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Awali, Bashungwa alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Vilevile, Rais Samia amemteua Angela Jasmine Kairuki kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kairuki ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Taarifa hiyo imeeleza kuwa mawaziri wote walioteuliwa wataapishwa leo – Oktoba 3, 2022, saa 3:00 asubuhi, Ikulu Jijini Dar es Salaam.

# ‘Ndoto za Alinacha’ Sekta ya Utalii

*Inatoka Uk. 11*

**Vikwazo kwenye njia za kupitia?**

Vikwazo vinavyoikabili sekta ya utalii ni pamoja na miundombinu duni ya utalii, wingi wa tozo kwa wawekezaji binafsi, ukosefu wa hoteli bora na za kutosha, uchache wa viwanja vya ndege; upungufu wa nguvu kazi mahiri; na uhaba wa matangazo ya vivutio kwa watalii wa ndani na nje.

**Nini kinafanyika sasa?**

Pambazuko limeelezwa kwamba wizara husika imeweka mikakati kadhaa kwa ajili ya kukwepa vikwazo na hivyo kufikia dira yake ya mwaka 2025.

Katika mwaka fedha 2022/2023, wizara inasema itakamilisha mkakati wa utekelezaji wa sera ya taifa ya utalii ya mwaka 1999; itaandaa programu ya maendeleo ya utalii nchini.

Katika hatua za kuendeleza mazao ya utalii nchini, wizara inaeleza kwamba itabainisha maeneo ya fukwe katika maziwa makuu ya Viktoria, Tanganyika na Nyasa kwa ajili ya uwekezaji na uendelezaji wa shughuli za utalii.

Aidha, Wizara itapanga huduma za malazi katika daraja za ubora katika mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya na Mwanza. Vilevile, wizara itatoa mafunzo kwa wadau wa utalii kuhusu matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora.

Wadau wa utalii na uchumi wanashauri kwamba wakati umefika sasa kwa Rais Samia kuhakikisha anasimamia vyema sekta ya utalii kwani pekee inaweza kuchangia sehemu kubwa ya mapato ya nchi na kuacha “kukamua wananchi wa kawaida” kwenye tozo na kodi lukuki.

Aidha, wanaeleza kwamba ni muhimu kupanua huduma za matangazo ya utalii nje ya Afrika, kwa kutumia vituo vikubwa vya televisheni.

Wanashangaa kwamba hadi sasa tovuti za kukuza utalii Tanzania hazina taarifa kadhaa za kuitangaza nchi, ikiwamo kukosekana kwa filamu ya “Tanzania-The Royal Tour” kwenye tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii wala tovuti ya Bodi ya Utalii Tanzania.

# Faida za uraia pacha

**Na Godwin CHILEWA**

KAWAIDA, suala la haki huenda sambamba na wajibu. Kwa kadri serikali itakavyoonesha kuwatendea haki Watanzania wanaoishi na kufanya kazi nje ya nchi (diaspora), ndivyo wengi watakavyovutwa na sheria, hivyo kulazimika kubeba wajibu unaoambatana na haki za "uzawa."

Kinyume na hivyo, wanadiaspora wengi wanaweza wasione haja au umuhimu wa kuwa sehemu ya watu wenye Hadhi Maalum hasa endapo sheria yenyewe itaonekana imetungwa ili kuwakomoa badala ya kuwasaidia.

Baadhi ya mambo ambayo serikali inaweza kufaidika na sheria ya kuwepo kwa uraia pacha ni pamoja na; kutoza kodi ya maendeleo.

Wajibu huo huwa mkubwa zaidi kwa mtu mwenye uraia pacha kwani hulazimika kulipa kodi katika nchi zote mbili alizo na uraia - kutegemea vitega uchumi na mapato yake.

Hata hivyo, serikali haitakuwa na haki ya kuwatoza kodi hiyo kama sheria ya Hadhi Maalum itapitishwa kama serikali inavyoelezwa kupendekeza, hivyo kuwapa haki nusunusu, na au wataingia nchini kwa kulipia viza kama wageni wengine.

Pia kwa uraia pacha, serikali itakuwa na uhakika zaidi kwa nchi kupata wawekezaji wa kilimo, viwanda na biashara ambao ni wazawa wa Tanzania.

Wako Watanzania wengi wenye uwezo mkubwa wa kifedha, mitandao ya biashara na uwekezaji, na uwezo wa kupata mitaji mikubwa huku nje ya nchi waliko, lakini wanasita kuwekeza nchini kwa hofu mbalimbali, ikiwamo kudhulumiwa.

Zaidi sana, nchi itakuwa na fursa ya kutumia wataalam wabobevu walioko nje, kwani maelfu ya Watanzania wenye elimu na uzoefu wa kimataifa wamejaa sehemu mbalimbali duniani.



***Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Tanzania, Dkt. Anna Makakala***

Baadhi yao wataalam hao wameajiriwa katika serikali, kampuni, na mashirika makubwa yanayoheshimika duniani, hawa wanaweza kuja ama kushirikiana na wenzao kusaidia mambo mengi ya kitaalamu kwa maendeleo ya Tanzania na watu wake.

Ni vyema sasa, serikali kupitia wizara ya mambo ya nchi za nje ifanye utafiti wa kina na kutilia maanani mapendekezo ya wanadiaspora ili sheria itakayoundwa iweze kuwa na manufaa kwa pande zote mbili.

Kinyume na hapo, kuna uwezekano mkubwa, endapo umakini na utayari wa kupisha sheria ya uraia pacha, Tanzania kuendelea kushuhudia nchi zingine, hasa za Kenya, zikifaidi uwepo wa sheria hiyo huko – kwa mchango unaotolewa na wananchi wake walioko nje.

***Mwandishi wa makala haya ni Mtanzania anayeishi na kufanya shughuli zake, Texas, Marekani.**

# Mtaka hataki ujinga Njombe

**Na Shabaan LULELA**

UJINGA ni mzigo, siyo kwa familia tu, bali jamii na taifa, Nchi yenye watu wajinga, maisha hugeuka kitanzi kwa wengi na mzigo mzito kwa serikali kuhudumia.

Ni kutokana na ukweli huo, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, anataka kuona watu wa mkoa wake wanaachana na ujinga, ambao ni chanzo kikubwa cha ufukara.

Tangu kuanza majukumu ya ukuu wa mkoa huo ulioko maeneo ya nyanda za juu kusini mwa Tanzania, Mtaka amekuwa akikomaa kuhimiza watendaji wenzake na wananchi kuanza kukataa ujinga kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Mtaka hataki kuona wanafunzi wanafanya vibaya darasani, kwenye mitihani ya kikanda na kitaifa na zaidi sana anataka kuona wanakuwa na uelewa na siyo kukaririshwa masomo.

Katika kuhakikisha hilo, amehimiza wanafunzi kusoma kwa bidii wanayofunzwa darasani, kujituma kazi za shule, kuheshimu walimu, wazazi, na kila mtu bila kujali rika.

"Elimu bora ni chanzo cha maarifa, ukiwa na elimu, maana yake unapiga hatua za kuyatambua mazingira na namna ya kupambana nayo- kwa njia hiyo unaanza kuachana na ufukara," anasema Mtaka.

Sambamba na kuwataka wanafunzi kuondoa ujinga, anawataka walimu kufanya kazi kwa bidii na kuona namna nzuri za kuongeza muda wa kufundisha darasani na hata nje ya darasa.

Kiongozi huyo anaweka bayana msimamo wake kwamba hatakasirika kuona mwalimu anafundisha vijana nje ya muda wa shule kwa maana ya masomo ya ziasa – maarufu tuisheni.

Kwamba kwa njia ya tuisheni, wanafunzi watasoma na kujifunza zaidi, huku walimu nao wakiongeza kipato chao kama ilivyo kwa watumisi wa kada zingine kama madaktari.



*Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka*

"Mimi nataka mfundishe zaidi, fundisheni wanafunzi mkiwa na muda wa ziada, kama umemaliza muda wangu wa serikali darasani na bado kuna uhitaji wa kufundisha, nenda kafundishe tuisheni, akija mtu yoyote kukuliza mwambie RC ameruhusu," anaongeza Mtaka.

Mtaka anasema hataki kuona mwalimu yeyote akifa kwenye ufukara, kwani wana fursa nzuri ya kupata fedha za ziada kwa kugawa ujuzi wa elimu kwa wanafunzi kwa malipo nafuu.

Mtaka anasema hapendi kuona mkoa wake ukikosekana kwenye nafasi nzuri za juu katika jedwari la ushindi katika matokeo ya kidato cha pili, nne na sita.

Kiongozi huyo, mbali na suala la elimu ambalo ni moja ya vipaumbele vyake anapenda kuona uchumi wa mkoa huo unapaa na kufika viwango vya juu; kwa kila mwananchi kuwa na maisha ya uhakika wa chakula cha kutosha, tiba na mahitaji mengine muhimu.

Anataka kubadili changamoto ya baridi kali, inayopatikana Njombe kugeuka kuwa fursa. Sasa yuko mbioni kuitangaza baridi kuwa moja ya vivutio vya utalii kwa watu wanaopenda hali hiyo ya hewa.

"Baridi sasa isionekane kuwa changamoto, bali tuitangaze na iwe kivutio. Watu watakuja kutalii hapa na kuona barafu, hawana haja ya kwenda Ulaya kushuhudia haya," anasema Mtaka.

# Mtawa atamani kufa haraka

**Na Tryruckia MFINANGA**

MWAKA jana aliambukizwa ugonjwa wa Covid-19, lakini alipona baada ya kuwa kwenye uangalizi na dawa kadhaa za kupunguza makali ya janga hilo lililosumbua dunia kwa karibu miaka mitatu.

Kutokana na umri wake, wengi waliamini mtawa wa Kanisa Katoliki (RC), Lucile Randon – akiwa na miaka 118, angepoteza maisha, kwani alikuwa mnyonge. Alishindwa kula wala kunywa vyema na ngozi yake 'ilinyauka' na kuonekana kama haijashikana na nyama.

Kupona kwa nyanya huyo, ambaye sasa anaaminika kuwa mwanamke mwenye umri mkubwa zaidi duniani, kuliwapa wanasanyansi wa tiba kwamba hata wenye umri mkubwa wanaweza kuambukizwa na wakapona Covid-19; siyo lazima wapoteze maisha.

Hata hivyo, baada ya kupona, sasa anatamani kufa kwani hana raha tena ya kuishi baada ya kueleza kuwa hana rafiki. Kwamba marafiki zake wote wamefariki dunia.

Nyanya huyo ambaye sasa haoni na hasikii vyema, akihojiwa hivi karibuni na mwandishi wa CBS, anasema siri ya kuishi miaka mingi namna hiyo ni "kufanya kazi." Anaongeza kwamba kabla ya kupatwa na changamoto za afya kutokana na umri, alikuwa akiendelea kufanya kazi zake za kuhudumia kanisa na familia ambazo zilihitaji msaada wa watawa.

"Nilikuwa nafanya kazi zangu hadi nilipokuwa na miaka 108, lakini baada ya hapo, afya yangu ikaanza kuleta mgogoro, kila mara naenda hospitali na nguvu za mwili kuniisha kwa haraka, ndipo sasa nikaacha kazi zangu," anasema bibi huyo.

Hivi sasa anaishi katika nyumba ya kulelea wazee katika Jiji la Toulon, ufukweni mwa Bahari ya Mediteranian, akiwa na changamoto ya kutembea pia. Anatumia baiskeli ya wagonjwa ya matairi manne ili kujongea.



*Bibi Andre (Picha na AFP-Image Gates)*

Anaeleza pia siri nyingine ya kuishi maisha marefu yenye furaha ni kusaidia jamii zenye uhitaji. Anasema; "idadi kubwa ya watu wenye kujitolea kusaidia wengine, huishi muda mrefu, ikiwa ni zawadi ya matendo yao mema."

Nyanya huyo ambaye ni maarufu zaidi nchini Ufaransa kwa jina la "Bibi Andre," amekuwa akipokea wageni wengi mashuhuri ambao humtembelea, hasa siku za sikukuu kwa kumjulia hali na wengine wakimpelekea zawadi lukuki.

Wengi wanaomtembelea nyanya huyo humpelekea peremende, chokoleti, ingawa amekuwa akipata tabu kumung'unya, ingawa ni mpenzi zaidi wa vitu hivyo vitamu.

Bibi Andre ambaye pamoja na changamoto za afya, bado hudamka alfajiri na kusukumwa hadi ndani ya kanisa kwa ajili ya kusali, amekuwa akisikitika kwa kushindwa kufanya kazi zake za kusaidia jamii; hasa wanawake na watoto.

***Makala haya yameandikwa kutoka vyanzo mbalimbali kutoka vyumba vya habari vya Ufaransa na Uingereza.***

# ‘Upelelezi wa kesi uharakishwe’

**Na Mwandishi WETU**

RAIS Samia Suluhu Hassan amekuwa akitoa maelekezo na matamko mengi kwa taasisi, jamii, kampuni na hata idara nyeti za taifa, huku baadhi ya wadau wakieleza wasiwasi wa kutoridhishwa na utekelezaji wake.

Baadhi ya wadau hao; wananchi, vyama vya siasa na hata mashirika ya kutetea haki za binadamu na wanasheria, wanadhani kuwa Rais Samia anapaswa kuongeza “ukali” kidogo kwa watendaji wake ili maagizo anayotoa yaonekane kutekelezwa.

Hivi karibuni Rais Samia aliagiza idara zote zinazohusiana na upelelezi wa mashauri mbalimbali kuhakikisha kwamba zinafanya upelelezi na kuwa na ushahidi wa kutosha kabla ya kumkamata mtuhumiwa na kumweka mahabusu.

Hii imekuwa moja ya kero kubwa kwa taifa, kwani kumekuwa na kucheleshwa kwa haki na wakati mwingine vyombo vinavyohusika na kesi, kuonea wahusika.

Rais alitoa agizo hilo Agosti 30, mwaka huu mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro wakati anafungua kikao kazi cha maofisa waandamizi wa Jeshi la Polisi kutoka makao makuu na makamanda wa mikoa na vikosi maalum.

Agizo hilo la Rais Samia lilipongezwa na kuungwa mkono na wananchi wengi, akiwamo Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Dkt. Edward Hoseah ambaye alisema mtu hastahili kupelekwa mahakamani kama upelelezi haujakamilika.

Dkt. Hoseah alisema madhara ya kumpeleka mtu mahakamani kabla ya upelelezi kukamilika ni pamoja na kumuumiza kwa kumharibia heshima yake na kuifanya familia kuishi kwa mashaka.

Hata hivyo, tangu kutolewa kwa agizo hilo, kuna wasiwasi kwamba hatua za kukamata watu wanaotuhumiwa kwa makosa kadhaa, bado zinaendelea zilezile za “kukamata kwanza na upelelezi baadaye.”



*RAIS Samia Suluhu Hassan*

Kutokana na hali hiyo, Shirika la Kutetea Jamii na Kutoa Misaada ya Kisheria (Cilao) limeamua kuingilia kati na kuhimiza kuanza kutekelezwa kwa agizo hilo la Rais Samia.

Shirika la kutetea na kutoa msaada wa kisheria (Cilao) linaeleza kwamba licha ya kauli hii ya Rais Samia kutaka kuzingatiwa kwa heshima, hifadhi na ulinzi wa haki za binadamu, bado kumekuwepo na changamoto ya utekelezaji wake.

Shirika hilo linaitaja Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka na idara zingine kuhakikisha inazingatia sheria na maagizo ya Rais Samia ili kuepuka kuonea watu.

Hivyo, Cilao kwa kushirikiana na wadau wa haki za binadamu nchini wameanza kukusanya taarifa za kesi zilizoko mahakamani kwa muda mrefu bila kusikilizwa kwa kile kinachoelezwa kwamba upelelezi haujakamilika.

Wananchi wanaombwa kutoa taarifa hizo kwa kujaza dodoso kupitia hapa: ***https://forms.gle/z8U2tJgKjjCyhPK18*** ili kujenga msingi wa kutekelezwa na kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati.

# Kipi muhumu zaidi kudhibiti Covid-19; chanjo au maombi?

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA ni miongoni mwa nchi kadhaa, hasa za Afrika ambazo kiongozi wake wa wakati huo, Rais John Magufuli aliamini kwamba maambukizi ya ugonjwa wa mfumo wa hewa; Covid-19 yanazuiwa kwa maombi kwa Mungu.

Rais Magufuli ambaye sasa ni marehemu, aliaminisha Watanzania kwamba kuwepo kwa ugonjwa huo ni nguvu za shetani, hivyo - kwa imani, haziwezi kushinda Nguvu za Mungu. Akawaasa wananchi kufunga na kusali ili kuuondoa ugonjwa huo.

Hata hivyo, imani hiyo inapingana na sayansi, ingawa kila mtu binafsi anabaki na kile anachoona kwake kina umuhimu. Wapo walioendelea na maombi, huku wakitumia "dawa" na wengine wakiacha kimoja.


Hivi karibuni, Afrobarometer, taasisi ya uchunguzi inayofuatilia takwimu Afrika, ilifanya utafiti na kubaini kuwa siyo Tanzania tu iliyokuwa na imani hiyo, bali nchi nyingine nyingi za bara hilo.

Ilibaini kwamba asilimia 22 ya Waafrika wote- wanaokadiriwa kufikia bilioni 1.4 hadi kufikia Oktoba Mosi, 2022 (Worldometer) walikuwa wamepata chanjo ya Covid-19.

Afrobarometer katika utafiti wake uliofanyika 2020/2021 ilibaini kwamba asilimia 57 ya hao asilimia 22; ambao ni watu wazima kuanzia miaka 20, kutoka nchi 16, walisema wanaamini zaidi maombi yalikuwa na matokeo bora zaidi kuliko chanjo ya kuzuia maambukizi ya Covid-19.

Utafiti huo ulibaini pia kuwa asilimia 24 walisema chanjo ni bora zaidi kuliko maombi, huku asilimia 16 wakieleza kuwa "maombi, lazima yaende sambamba na chanjo."

Upendeleo wa maombi ulikuwa karibu kwa wote nchini Niger (88%), Sudan




(87%), na Liberia (86%). Benin – wao wakiamini zaidi tiba za jadi (50%).

Ilibainika kuwa katika nchi hizo, asilimia 71 ya watu fukara (wenye kuhangaika hata kula mlo mmoja kwa siku) waliamini zaidi katika maombi, huku asilimia 61 ya wasiokuwa na elimu ya msingi wakiamini kwenye maombi zaidi katika kuikabili Covid-19.

# Una mimba? Tafuna karanga

**Na Dkt. Isamile MAGENA**

Mwenye ujauzito ni maneno yanayotumika kumtambulisha mwanamke aliyebeba kiumbe kingine tumboni. Ni yule mwenye mimba ambaye – kwa kawaida, hulea mimba hiyo kwa miezi tisa kabla ya kujifungua na kuleta binadamu mwingine kwenye uso wa dunia.

Katika mazingira hayo, mwanamke huyo anakuwa analea binadamu mwingine ndani ya mwili wake, hivyo kuhitaji maisha maalum ili kujenga makuzi ya kiumbe kilichomo tumboni mwake.

Wakati wa ujauzito, mwili wa mwanamke unahitaji kuwa na damu ya ziada ili kusaidia ukuaji wa mtoto uwe thabiti na wenye uhakika. Na damu, haiongezwi kwa kuwekewa damu kila mara hospitalini, bali kunahimizwa kula vyakula vingi vyenye madini ya chuma, ambayo ni kiungo muhimu zaidi kutengeneza damu kwenye mwili.

Bila madini ya chuma ya kutosha, mwili wa mwanamke mwenye ujauzito, hushindwa kugawa damu ya kutosha kwake mwenyewe na hata kwa mtoto,hivyo kushauriwa kula nafaka, hasa karanga ambao zimethibitika kisayansi kuwa na madini mengi ya chuma.

Kupungua kwa damu mwilini husababisha kuwepo kwa ugonjwa unaoitwa kitaalam – Anemia, hivyo ili kukabiliana na hatari hii, ni lazima wanawake wajawazito wahakikishe wanapata karanga, tena zikiwa mbichi, kwa kiwango cha kutosha.

Karanga ni chanzo kikubwa cha madini ya chuma, ndiyo maana inashauriwa kwamba wanawake wenye mimba watafune zaidi karanga mbichi ili kuepuka upungufu wa damu kwake na hata kwa mtoto aliyemo tumboni.

Mbali na kuongeza damu, karanga (na hata nafaka zingine kama korosho) imethibitika kitaalamu kuwa na kiasi kikubwa cha madini ya Zinki (Zinc) ambayo ni muhimu zaidi kukomaza ubongo wa mtoto anapokuwa tumboni.



*Mtoto akiwa tumboni (Picha ya ASN)*

Imebainika kuwa wanawake wenye ujauzito kuanzia wiki nne hadi sita, ni muhimu sana wakaweka mazoea ya kutafuna karanga mbichi (na hata korosho mbichi) kwa kuwa zina virutubisho vinavyoitwa ‘folate’ ambavyo kazi yake kubwa ni kukuza na kuimarisha uti wa mgogo kwa mtoto mchanga, hasa akiwa tumboni.

Mara nyingi wanawake wajawazito – kwa idadi kubwa hukabiliwa na tatizo la kuwa na choo kigumu, hivyo kutafuna karanga ni tiba nzuri zaidi kwani hulainisha choo na kuondoa usumbufu wa ‘kujikamua’ kila anapoenda haja.

Pamoja na faida hizo kwa mama wajawazito, pia karanga mbichi na hata korosho, hutumika zaidi kwa watu wanaopenda kupunguza uzito, bila kulazimika kufanya mazoezi kila mara, kwani kutafuna nafaka hizo huondoa njaa, hivyo kumpunguza mhusika kula-kula, kila mara. Na kwa njia hiyo, kuongeza kasi ya mwili kuchoma mafuta yasiyohitajika mwilini.

***Mwandishi amejitambulisha kuwa mtaalamu wa lishe na tabibu anayeishi Tabora.***

# Tutakumbuka daima...



***Kwamba Balozi Getrude Mongela alikuwa kiongozi wa mkutano mkubwa wa dunia wa wanawake uliofanyika Beijin, China mwaka 1995. Baada ya mkutano huo maarufu, Balozi Mongela alipata wasaa wa kwenda kukutana na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) wakati huo, Boutros Ghali kwenye makao makuu ya umoja huo, New York , Marekani (Picha kutoka Maktaba ya Pambazuko).***



*1. Bwana Harusi, Tajiel Urioh ambaye ni Mshauri wa Nishati, Ubalozi wa Norway Tanzania na Bibi Harusi, Wakili Subira Mwambile wakiwa wakifurahi baada ya kukamilisha taratibu za ndoa na sasa ni mke na mume.*

*2. Maharusi wakiwa na anamichezo wenzao wa baiskeli kutoka Klabu ya Twende Butiama baada ya harusi iliyofungwa Kanisa la Azania Front, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.*

*3. Bwana na Bibi Harusi wakiwa na Wanamichezo wenzao wa baiskeli kutoka klabu yao baada ya harusi. (Picha zote na Mkuya Media)*





# Mabadiliko ya teknolojia duniani



**Na Mwandishi WETU**

KILA mahali duniani kwa sasa, wimbo wa uchumi wa kidijitali ndiyo unaotawala habari na mazungumzo ya maendeleo.

Ni wimbo wenye historia ndefu ambao kuimbwa kwake hauwezi kukoma kwani huenda ukibadilika kutokana na sababu mbalimbali za kukua kwa sayansi.

Mwanadamu amepitia awamu nyingi za mabadiliko ya maisha yake kutokana na makuzi ya mifumo ya maisha na mazingira.

Alianzia kwa kuwinda na kukusanya matunda kwa ajili ya chakula chake, lakini miaka ya 1500KK akaachana mfumo huo na akawa mfugaji.

Baadaye, kwenye miaka ya 800BK, akaachana na ufugaji wa kuhamahama na kuwa mkulima mwenye makazi maalum. Akawa mkulima anayetumia zana duni kama vile jembe la mkono.

Na hatimaye, katika miaka ya 1700BK akaachana na ukulima na kuwa mfanyakazi wa viwandani. Huku akawa mtumiaji wa mashine zinazorahisisha kazi. Uzalishaji ukapanda, utajiri mkubwa ukazaliwa kutokana na uzalishaji wa ziada.

Na kwa muda wa miaka 300 ambayo binadamu amefanya kazi za viwandani, amepitia katika mapinduzi ya viwanda ya awamu nne, kila awamu ikiwa na upekee wake.

Awamu ya kwanza ya mapinduzi ya viwanda, iliyotokea miaka ya 1760, ilisifika kwa mitambo iliyotumia nishati ya mvuke wa maji.

Awamu ya pili ya mapinduzi ya viwanda, iliyotokea miaka ya 1900, ilisifika kwa mitambo iliyotumia nishati ya petroli na umeme.

Awamu ya tatu ya mapinduzi ya viwanda, iliyotokea miaka ya 1900, ilisifika kwa mitambo iloyotumia vifaa vya kielektroniki, kama vile simu na kompyuta.

Kila hatua ya mapinduzi ya kiuchumi na kijamii iliambatana na upekee wake katika sayansi na teknolojia ya uzalishaji wa mali.

Kila awamu ikiwa na sayansi na teknolojia bora zaidi kuliko awamu iliyotangulia; na kila awamu ikiwa inapata somo kutokana na makosa yaliyofanyika kwenye awamu za nyuma.

Kwa hiyo, ustaarabu wa dunia ya leo ni matunda ya fikra za mnyororo mrefu wa wanasayansi na ule wa teknolojia uliotangulia.

Kwa ufupi, mchango wa wanasayansi na wanateknolojia hawa katika ulimwengu wa leo ni imani ifuatavyo:

Kwamba, ushahidi unaotokana na utafiti unapaswa kuaminika zaidi kuliko ushahidi unaotokana na matamko ya watawala.

Kwamba, mfumo wa ulimwengu unaongozwa na kanuni za maumbile zenye kuunganisha vitu vyote vilivyomo ulimwenguni kwa kutumia kanuni ya sababu na matokeo, pasipo mkono wa miungu.

Kwamba, katika uhusiano wowote wa sababu na matokeo, sababu huwa na

# Alama asilia na ubunifu wa watu

**Na Deusdedith KAHANGWA**

MAWAZO kwamba, "kitu kilichowahi kuwa sababu ya matokeo fulani huchukuliwa kama alama ya matokeo hayo," kama ambavyo, "mawingu ni alama ya mvua."

Haya ni mawazo ya mwanafalsafa aitwaye Charles Sanders Peirce (1839 - 1914), ninayejadili fikra zake leo.

Peirce alikuwa mwanafalsafa, mwanasayansi na mwanahesabu wa Marekani ambaye ni mwasisi wa taaluma ya "semiolojia," yaani "semiology" au "semiotics." Hili ni tawi la falsafa linalochunguza uhusiano uliopo kati ya alama, maana ya alama na akili ya mtumia alama.

Atakumbukwa zaidi kwa sababu ya mafundisho yake kwamba, alama zote zinazofahamika duniani zinaweza kugawanywa kwenye makundi matatu bila kubaki. Hizo ni "alama elekezi, alama simbolika na alama ikonika." Nitaeleza aina hizi kwa kifupi.

Kwanza, kwa mujibu wa maandiko ya Peirce, "alama elekezi," yaani "indexical sign," ni alama inayobeba maana kwa sababu ya uhusiano asilia uliopo kati ya alama yenyewe na kitu kinachowakilishwa. Kwa mfano kuna uhusiano asilia kati ya sababu na matokeo yanayoletwa na sababu hiyo.

Hivyo, katika mazingira fulani, "sababu ni alama ya matokeo." Kwa mfano, mawingu ni alama ya mvua, tendo la ngono ni alama ya mimba inayoweza kutokea, jua ni alama ya kiangazi, na hasira ni alama ya ugomvi unaoweza kutokea.

Na katika mazingira mengine, "matokeo ni alama ya sababu." Kwa mfano, moshi ni alama ya moto, kicheko ni alama ya furaha, kilio ni alama ya huzuni, kufoka ni alama ya hasira, mwangwi ni alama ya sauti ya kitu fulani, mimba ni alama ya tendo la kujamiiana, na orodha inaendelea.

Pili, kwa kuzingatia mawazo ya Peirce, "alama ikonika," yaani "iconic sign," ni alama inayofanana na kitu inachokiwakilisha.


*Charles Sanders Peirce*

Kwa mfano, picha ya mtu, picha ya kitu, alama ya daraja kwenye somo la jiografia, alama ya barabarani inayoonyesha mteremko mkali, mchoro wa jengo, ramani ya shule, na alama zinazotumika kwenye maeneo mbalimbali.

Na tatu, kulingana na maandiko ya Peirce, "alama simbolika," yaani "symbolic sign," ni alama inayowakilisha kitu kwa sababu kuna kikundi cha watu kimeamua hivyo, japo hakuna ufanano wowote kati ya alama na kitu kinachowakilishwa na alama husika. Inabeba maana iliyochaguliwa kiholela na mtu.

Kwa mfano, bendera ya taifa, nembo ya taifa, msalaba unaowakilisha Ukristo, mwezi na nyota vinavyowakilisha uislamu, msalaba mwekundu unaowakilisha kazi ya uokoaji, na nembo za kampuni mbalimbali.

Kwa hiyo, ukaribu kati ya alama na kitu kinachowakilishwa unapungua kadiri tunavyotoka kwenye "alama elekezi" kupitia kwenye alama ikonika" na kusogea kwenye "alama simbolika."

Jambo kubwa hapa ni kwamba, "alama elekezi" ni alama inayobeba maana asilia. Kwa hiyo, tunaposema kuwa, baadhi ya taasisi za kijamii ni "taasisi asilia," tunamaanisha kuwa zinatambulishwa na "alama elekezi," ambazo kwa mujibu wa Peirce ni "alama asilia."

# Salima: Muuguzi Rwanda kupuliza kipyenga Kombe la Dunia Qatar

**Na Mwandishi WETU**

ZIKIWA zimebaki siku 49 kufikia Novemba 21, mwaka huu, macho na masikio ya wapenzi wa soka "yatahamia" Qatar ambako mtanange wa Kombe la Dunia utaanza.

Pamoja na idadi kubwa ya wapenzi hao kujiandaa kufuatilia wachezaji wanaowapenda na kuangalia mechi za michuano hiyo mikubwa zaidi ya soka duniani, lakini pia watakuwa na wasaa wa kupima uwezo wa wanawake katika nafasi ya uamuzi wa mpira wa miguu.


Zaidi sana, wengi wamejipanga kutazama uamuzi wa mwanamama Mwafrika wa kwanza kuwa mwamuzi wa kati tangu kuanza kwa michuano hiyo miaka 92 iliyopita baada ya aliyekuwa Rais wa Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) – wa wakati huo, Jules Rimet kuja na wazo hilo.

Mwanamke huyo Salima Rhadia Mukansanga (33)– raia wa Rwanda aliyegeuka gumzo baada ya kutangazwa na FIFA kwamba atapuliza kipyenga katika michuano hiyo, anatarajiwa kutenda kinyume na matarajio ya wengi, hasa wenye kushabikia mfumo dume, wanaoamini soka ni kwa ajili ya wanaume.

Imani ya wengi kwamba Salima ataweza, inatokana na kupitia "tanuri" kubwa katika mchakato mzima wa kumpitisha hadi kufikia hatua hiyo.

Jina la Salima lilitajwa miongoni mwa waamuzi 129 waliopitishwa kuwa waamuzi katika kombe hilo linaloanza Novemba 21 na kukamilika Desemba 18, mwaka huu ambapo bingwa wa soka wa dunia atapatikana. Anaungana na wanawake wengine watatu, wote wakitokea nchi za Ulaya.

Pierluigi Collina, Mkuu wa Kamati ya Waamuzi ya FIFA, anasema kwamba ana imani kubwa na Salima kwa kuwa amekuwa akishiriki katika mchujo mkali wa kuwapata waamuzi na katika kipindi chote ameonyesha "uwezo wa ajabu."



*Salima Rhadia Mukansanga*

Akiwa msomi mwenye shahada ya kwanza ya uuguzi na ukunga, Salima anasema tangu akiwa binti, alipendelea zaidi michezo, na hasa mpira wa kikapu, lakini kadri alivyokuwa akikua mapenzi yake yakageukia mpira wa miguu.

"Nilitambua mchezo huo ni wa wanaume zaidi, baadaye nikapata wazo la kuwa mwamuzi, nikipenda zaidi kusimamia sheria na taratibu za wanaume wanapocheza uwanjani," alisema Salima.

# PICHA KUBWA



*Mmoja wa ndege wazuri wanaopatikana katika Hifadhi ya Taifa ya Kitulo, Njombe. Ndege huyo ambaye anaaminika kuwa na rangi saba, ni maarufu kwa kudonyoa maua. (Picha ya Mtandao).*

*GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.*